# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
# OFISI YA MBUNGE, JIMBO LA MUSOMA VIJIJINI

# UTEKELEZAJI WA ILANI YA UCHAGUZI YA CHAMA CHA MAPINDUZI (2015-2020)

## *(TAARIFA YA JULAI 2019 - JUNI 2020)*

*VOLUME II*

**JUNI 30, 2020**

## YALIYOMO

## Contents

YALIYOMO ........................................................................................................0

1. UTANGULIZI ..................................................................................................5

2. SEKTA YA ELIMU ..........................................................................................6

2.1. KUFUNGULIWA KWA SEKONDARI MPYA ..............................................6

2.2. SEKONDARI MPYA ZINAZOJENGWA .......................................................8

2.3. VYUMBA VIPYA VYA MADARASA ........................................................10

2.4. UJENZI WA MAKTABA ..........................................................................12

2.5. UJENZI WA SHULE SHIKIZI ....................................................................13

2.6. MIRADI YA SERIKALI KWENYE SEKTA YA ELIMU ............................15

2.6.1. EDUCATION QUALITY IMPROVEMENT PROGRAMME (EQUIP) ....15

2.6.2. EDUCATION PROGRAMME FOR RESULTS (EP4R) ............................15

2.6.3. UGAWAJI WA VITABU VYA SAYANSI NA KIINGEREZA ................15

3. SEKTA YA AFYA .........................................................................................16

3.1. ZAHANATI ZINAZOTOA HUDUMA ZA AFYA .......................................16

3.2. ZAHANATI MPYA ZINAZOJENGWA NA WANAVIJIJI ..........................17

3.3. UJENZI WA WODI ZA MAMA NA MTOTO .............................................18

3.4. VITUO VYA AFYA.....................................................................................19

3.4.1. VITUO VYA AFYA VINAVYOTOA HUDUMA .....................................19

3.4.2. KITUO CHA AFYA KIPYA ......................................................................19

3.4.3. HOSPITALI YA WILAYA........................................................................20
4. SEKTA ZA KILIMO, UVUVI NA UFUGAJI ..................................................20
4.1. KILIMO ..................................................................................................21
4.1.1. PLAU ....................................................................................................21
4.2. UVUVI....................................................................................................22
4.3. UFUGAJI................................................................................................22
5. MAZINGIRA............................................................................................22
6. UTAMADUNI NA MICHEZO.....................................................................23
7. MICHANGO YA WADAU WA MAENDELEO...............................................24
7.1. PROJECT CONCERN INTERNATIONAL (PCI).........................................24
7.2. BMZ .......................................................................................................25
7.3. MICHANGO YA MABENKI.......................................................................26
7.4. JAMII IMPACT LIMITED .........................................................................27
7.5. WADAU WENGINE WA MAENDELEO......................................................28
7.5.1. JOHNS HOPKINS PROGRAM (JHPIEGO)................................................28
7.5.2. INTERNATIONAL CENTER OF AIDS (ICAP)...........................................28
7.5.3. ARIEL GLASER INITIATIVES (AGPAHI)..................................................29
7.5.4. AGRICULTURE FRONTIES TANZANIA (AFRO TANZANIA)............29
7.5.5. SWISSCONTACT......................................................................................29
7.5.6. MEDA ECONOMIC DEVELOPMENT ASSOCIATES (MEDA).............30

7.5.7. SHIRIKA LA MAENDELEO YA KILIMO (SHIMAKIUMU) ..................31
7.5.8. AFRICAN INLAND CHURCH OF TANZANIA (AICT)...........................32
7.5.9. VICTORIA FARMING AND FISHING ORGANIZATION (VIFAFIO)...32
7.5.10. MARIE STOPES .........................................................................32
7.5.11. POPULATION SERVICES INTERNATIONAL (PSI) .............................32
7.5.12. INTRAHEALTH INTERNATIONAL.......................................................33
7.5.13. JOHN SNOW INC (JSI).........................................................................33
7.5.14. CENTRE FOR WIDOWS AND CHILDREN ASSISTANCE (CWCA)...33
7.5.15. LAW SCHOOL ADMISSION COUNCIL (LSAC) ...................................33
7.5.16. CHRISTIAN COUNCIL OF TANZANIA (CCT).....................................33
7.5.17. WORLD EDUCATION INC (WEI) .........................................................35
7.5.18. ONE WORLD SUSTAINABLE LIVELIHOOD (OWSL).........................36
7.5.19. CHAMA CHA UZAZI NA MALEZI TANZANIA (UMATI)...................36
7.5.20. KANISA LA KIINJILISTI LA KILUTHERI TANZANIA (K.K.K.T) .....36
7.5.21. UMOJA WA MAENDELEO YA WATU WA BUKWAYA (UMABU)..36
7.5.22. MUSOMA RURAL PARALEGAL ORGANIZATION (MRPO) .............37
7.5.24. SUSTAINABLE HUB FOR POLICY INITIATIVES (SHPI) ...................37
7.5.25. WATOTO WAPINGE UKIMWI................................................................37
7.5.28. TANZANIA RED CROSS .........................................................................37
7.5.29. SHIRIKA LA MAENDELEO UTAFITI NA TIBA (SHIMAUTITA) ......38

7.5.30. WAZALIWA WA JIMBO LA MUSOMA VIJIJINI................................38

8. MIRADI MINGINE YA MAENDELEO..........................................................38

8.1. MAJI ............................................................................................................39

8.1.1 MIRADI YA MAJI KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021.....................39

8.1.2 MIRADI MINGINE YA MAJI KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021 ..39

8.1.3 MIRADI MIKUBWA YA MAJI.................................................................40

8.2. UMEME VIJIJINI (REA)...........................................................................41

8.3. BARABARA ...............................................................................................41

8.3.1. UJENZI WA BARABARA YA LAMI (TANROADS) ..............................41

8.3.2. MATENGENEZO YA BARABARA (TANROADS)................................41

8.3.3. MATENGENEZO YA BARABARA VIJIJINI (TARURA)........................42

9. HUDUMA ZA BENKI VIJIJINI...................................................................42

10. USHIRIKI KWENYE SHUGHULI ZA CHAMA...........................................43

11. KUSHIRIKIANA NA MADHEHEBU YA DINI............................................44

12. USHIRIKI KWENYE MASUALA YA KIJAMII............................................45

13. HITIMISHO..................................................................................................45

14. SHUKRANI...................................................................................................46

KIAMBATANISHO NAMBA 2:.........................................................................51

## 1. UTANGULIZI

TAARIFA za Jimbo la Musoma Vijijini za Utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi (CCM) ya Mwaka 2015 – 2020 ni MBILI. Taarifa ya kwanza (Volume I) yenye kurasa 110 ilichapishwa tarehe 7 Julai 2019. Nakala 5,000 (elfu tano) zilichapishwa na kugawiwa bure kwa Wananchi wa Jimbo la Musoma Vijijini. Viongozi wa Vyama vya Siasa na Serikali wa ngazi zote (Vijiji, Kata, Wilaya, Mkoa na Taifa) nao waligawiwa bure nakala za taarifa iliyochapishwa tarehe 7 Julai 2019.

TAARIFA hii ya pili (Volume II) yenye nakala 5,000 (elfu tano) imechapishwa tarehe 30 Juni 2020, na kusambazwa bure kwa walengwa wote kama ile iliyotangulia (Vulume I).

Taarifa hii inaeleza muendelezo wa Utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM (2015 - 2020) kwenye Jimbo la Musoma Vijijini kwa kipindi cha mwaka mmoja (Julai 2019 - Juni 2020). Vilevile, Taarifa hii inaonesha MICHANGO mingi na mikubwa inayoendelelea kutolewa na Mbunge wa Jimbo, Prof Sospeter Mwijarubi Muhongo kwenye Utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM (2015 – 2020) ndani ya Jimbo la Musoma Vijijini. Kwa ujumla, Ilani ya Uchaguzi ya CCM (2015 – 2020) inaendelea kutekelezwa kwa mafanikio makubwa sana na hii inathibitisha jinsi ambavyo Serikali ya Awamu ya Tano chini ya Uongozi wa Mheshimiwa Rais Dkt John Joseph Pombe Magufuli inavyoendelea kuwaletea Wananchi maendeleo ya uhakika kwenye Jimbo la Musoma Vijijini.

Jimbo la Musoma Vijijini lenye jumla ya Kata 21, Vijiji 68, Vitongoji 374 na wakazi takriban laki tatu na nusu (350,000) limeendelea kutekeleza VIPAUMBELE vyake vitano (5) ambavyo ni (i) Elimu, (ii) Afya, (iii) Kilimo (Uvuvi na Ufugaji), (iv) Mazingira, na (v) Michezo na Utamaduni kama yalivyoainishwa kwenye Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi (CCM) ya Mwaka 2015 – 2020. Maji, umeme, barabara, vyombo vya usafirishaji na mawasiliano ni nyenzo muhimu zinazotumika kufanikisha Utekelezaji wa Miradi ya VIPAUMBELE hivyo vitano ili kuimarisha UCHUMI na USTAWI wa Wananchi wa Jimbo la Musoma Vijijini.

## 2. SEKTA YA ELIMU

### 2.1. KUFUNGULIWA KWA SEKONDARI MPYA

Kwa sasa (Juni 2020), Jimbo la Musoma Vijijini lina jumla ya Sekondari 20 (ishirini) za Serikali (Kata) na mbili za Binafsi (Private). Sekondari mpya zilizofunguliwa Januari 2020 ni:

i) Dan Mapigano Memorial Secondary School ya Kata ya Bugoji
ii) Busambara Secondary School ya Kata ya Busambara



*Moja ya majengo ya Vyumba vya Madarasa ya Dan Mapigano Memorial Secondary School iliyojengwa katika Kata ya Bugoji*



*Wanafunzi waliojiunga na Kidato cha kwanza katika Shule Mpya ya Sekondari ya Kata ya Busambara*

Jimbo la Musoma Vijijini limedhamiria kuwa na MAKTABA nzuri kwenye Sekondari zake zote, Mbunge wa Jimbo, Prof Sospeter Mwijarubi Muhongo anaendelea kupewa Vitabu vingi vya masomo ya Sayansi, Kiingereza, n.k kutoka Marekani na Uingereza. Kwa hiyo, ujenzi wa MAKTABA na MAABARA kwenye Sekondari zetu zote unawekewa msisitizo mkubwa na utekelezaji wake unaendelea.

## 2.2. SEKONDARI MPYA ZINAZOJENGWA

Wanavijiji kwa kushirikiana na Serikali yao, Mbunge wa Jimbo, Wazaliwa wa Jimbo hili na Wadau wengine wa Maendeleo, wameamua kujenga Sekondari mpya ili kutatua matatizo makubwa mawili:

(i) Umbali mrefu wanaotembea Wanafunzi kwenda masomoni, na
(ii) Mirundikano ya Wanafunzi kwenye vyumba vya Madarasa.

Sekondari mpya zinazojengwa zimepangwa kusajiliwa na kufunguliwa mwakani (Januari 2021). Sekondari hizo ni:

- (i) Kigera Secondary School ya Kata ya Nyakatende. Hii ni Sekondari ya pili ya Kata hiyo,
- (ii) Seka Secondary School ya Kata ya Nyamrandirira. Hii ni Sekondari ya pili ya Kata hiyo,
- (iii) Bukwaya Secondary School ya Kata ya Nyegina. Kata hii inazo Sekondari mbili – moja ya Serikali (Kata) na nyingine ya Kanisa Katoliki,
- (iv) Nyasaungu Secondary School, inajengwa na Kijiji kimoja tu cha Nyasaungu, Kata ya Ifulifu, na

(v) Ifulifu Secondary School inayojengwa na Vijiji viwili vya Kabegi na Kiemba, vyote vya Kata ya Ifulifu.



*Baadhi ya Wajumbe wa Serikali ya Kijiji cha Kigera na Wananchi wa Kijiji hicho wakikagua ujenzi wa Jengo la Maabara katika Sekondari Mpya ya Kigera inayojengwa Kijijini hapo*



*Mafundi wakiendelea na ujenzi wa Sekondari ya Seka inayojengwa na Vijiji vitano vya Chumwi, Kaboni, Kasoma, Mikuyu na Seka katika Kata ya Nyamrandirira*



*Wananchi wa Kata ya Ifulifu wakishirikiana na Mafundi katika ujenzi wa Sekondari ya Kata ya Ifulifu inayojengwa Kijijini Kabegi*

SHUKRANI nyingi zinatolewa kwa Mgodi wa Dhahabu wa Kijijini Seka (MMG) kwa kuchangia ujenzi wa Sekondari Mpya ya Kata ya Nyamrandirira inayojengwa Kijijini hapo.

Vijiji vya Wanyere (Kata ya Suguti), Busamba (Kata ya Etaro), Kurwaki na Nyang'oma (Kata ya Mugango) vinajitayarisha kuanza ujenzi wa Sekondari ya pili ya Kata zao.

## 2.3. VYUMBA VIPYA VYA MADARASA

Jimbo la Musoma Vijijini lina jumla ya Shule za Msingi 111 (mia moja kumi na moja) za Serikali na 3 (tatu) za Binafsi (Private).

Kutokana na matatizo ya umbali mrefu wa kutembea kwenda masomoni, na kuwepo kwa mirundikano mikubwa ya Wanafunzi kwenye vyumba vya madarasa (k.m. Wanafunzi 70 – 200 kwenye chumba kimoja), Wananchi kwa kushirikiana na Serikali yao, Mbunge wao wa Jimbo na Wadau wengine wa Maendeleo,

wameamua kujenga vyumba vipya vya madarasa kwa Shule zote za Msingi za Jimbo la Musoma Vijijini. Hadi kufikia Juni 2020, vyumba VIPYA vya MADARASA 530 vimeishajengwa na kutumika na vichache kati ya hivyo vinakamilishwa. Haya ni MAFANIKIO makubwa sana.



*Afisa Mtendaji wa Serikali ya Kijiji cha Kurwaki, Ndugu Abeid Makamba Ndagara akiwa katika viwanja vya Shule ya Msingi Karubugu vinapojengwa vyumba vipya viwili vya Madarasa*



*Wananchi na Viongozi wa Kijiji cha Kwikerege, Kata ya Rusoli wakikagua ujenzi wa vyumba viwili vya Madarasa katika Shule ya Msingi Kwikerege*

## 2.4. UJENZI WA MAKTABA

USHIRIKIANO mzuri wa Serikali yao, Viongozi wa Kata na Vijiji, Mbunge wa Jimbo la Musoma Vijijini, Wazaliwa wa Jimbo hili na Wadau wa Maendeleo unazidi kuzaa matunda mazuri kwenye ujenzi na uboreshaji wa Miundombinu ya Elimu ikiwa ni pamoja na ujenzi wa Maktaba kwenye Shule za Msingi. Hadi sasa, jumla ya Maktaba 3 (tatu) zinajengwa wakati Maktaba moja ya Rukuba Kisiwani imeshakamilika na tayari inatumika. Orodha ya Maktaba hizo ni:

(i) Maktaba ya Shule ya Msingi Rukuba, iliyojengwa kwa Michango ya Wananchi, PCI, Mbunge wa Jimbo na Serikali,

(ii) Maktaba ya Shule ya Msingi Butata inayojengwa kwa nguvukazi na Michango ya fedha kutoka kwa Wananchi, PCI, Mbunge wa Jimbo na Wazaliwa wa Butata,

(iii) Maktaba ya Shule ya Msingi Buraga inayojengwa kwa Michango ya Wananchi na PCI,

(iv) Maktaba ya Shule ya Msingi Busamba, iliyojengwa kwa Michango ya Wananchi, Mbunge wa Jimbo na PCI.



*Makataba ya Shule ya Msingi Rukuba iliyopo Kijijini Rukuba (Kisiwani) iliyojengwa kwa MICHANGO ya Wananchi, PCI, Mbunge wa Jimbo na Wadau wengine wa Maendeleo*



*Maktaba ya Shule ya Msingi Buraga iliyopo Kijijini Buraga ambayo inajengwa kwa MICHANGO ya Wananchi*

## 2.5. UJENZI WA SHULE SHIKIZI

Kutokana na msongamano wa Wanafunzi kwenye vyumba vya Madarasa ya Shule za Msingi, umbali mrefu wa Wanafunzi kutembea kwenda Vijiji jirani kupata Elimu ya Msingi, Wananchi

wa Jimbo la Musoma Vijijini kwa kushirikiana na Serikali na Mbunge wa Jimbo wameendelea na ujenzi wa Shule Shikizi 11 ambazo hadi sasa nyingine zimekamilika na tayari zimeanza kupokea Wanafunzi. Shule hizo ni:

- Binyago: inayojengwa Kijijini Kabegi, Kata ya Ifulifu
- Buanga: Kijijini Buanga, Kata ya Rusoli
- Buraga Mwaloni: Kijijini Buraga, Kata ya Bukumi
- Egenge: Kijijini Busamba, Kata ya Etaro
- Gomora: Kijijini Musanja, Kata ya Musanja
- Kaguru: Kijijini Bugwema, Kata ya Bugwema
- Karusenyi: Kijijini Mikuyu, Kata ya Nyamrandirira
- Kihunda: Kijijini Kamuguruki, Kata ya Nyakatende
- Mwikoko: Kijijini Chitare, Kata ya Makojo
- Rwanga: Kijijini Kasoma, Kata ya Nyamrandirira
- Ziwa: Kijijini Mwiringo, Kata ya Busambara



*Wananchi wa Kijiji cha Buanga wakijumuika pamoja na Viongozi wao wa Kata na Kijiji katika ujenzi wa Shule Shikizi ya Buanga*

## 2.6. MIRADI YA SERIKALI KWENYE SEKTA YA ELIMU

### 2.6.1. EDUCATION QUALITY IMPROVEMENT PROGRAMME (EQUIP)

MRADI wa EQUIP (The Education Quality Improvement Programme) unaboresha Miundombinu ya Elimu ikiwemo ya ujenzi wa vyumba vya Madarasa, Ofisi za Walimu, matundu ya vyoo vya Wanafunzi na Walimu, na ujenzi wa matenki ya kuvunia maji ya mvua. Wananchi wa Jimbo la Musoma Vijijini, wameendelea kushirikiana na Serikali yao kupitia Mradi huu wa EQUIP.

### 2.6.2. EDUCATION PROGRAMME FOR RESULTS (EP4R)

Huu ni MPANGO wa Kulipa Kulingana na Matokea unaolenga kuboresha kiwango cha Elimu kwa Shule za Sekondari nchini kote chini ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. Jimbo la Musoma Vijijini kupitia Halmashauri ya Wilaya ya Musoma limeendelea kutoa ushirikiano mkubwa kupitia MPANGO huu ambao umewezesha kujenga vyumba vya madarasa kwa Shule za Sekondari. Wananchi wa Musoma Vijijini wameendelea kuutambua na kuuthamini mchango mkubwa wa EP4R Jimboni mwetu.

Hadi kufikia Juni 2020, vyumba VIPYA vya MADARASA 150 vimejengwa. Haya ni MAFANIKIO makubwa sana.

### 2.6.3. UGAWAJI WA VITABU VYA SAYANSI NA KIINGEREZA

Mbunge wa Jimbo la Musoma Vijijini, Prof Sospeter Mwijarubi Muhongo ameendelea kugawa bure Vitabu vya Sayansi na Kiingereza kutoka Marekani na Uingereza. Baadhi ya Shule

zilizogawiwa Vitabu vya awamu hii ya tano ni Sekondari mpya ya Busambara, Sekondari mpya ya Kumbukumbu ya Dan Mapigano, Shule ya Msingi Agape (private) na kwa Wadau mbalimbali wa Elimu wakiwemo Wabunge kwa ajili ya Shule zao.

## 3. SEKTA YA AFYA

Mbunge wa Jimbo la Musoma Vijijini, Prof Sospeter Mwijarubi Muhongo ameendelea kuwashawishi Wananchi wa Jimbo la Musoma Vijijini waendelee kutekeleza Ilani ya CCM inayosema kila Kijiji kiwe na Zahanati moja na kila Kata moja iwe na Kituo cha Afya kimoja. Mbunge wa Jimbo pia ameendelea kushirikiana na Serikali, Wananchi Vijijini, Madiwani, Wazaliwa wa Jimbo hili, baadhi ya Wafanyabiashara Vijijini na Wadau wengiine wa Maendeleo kwenye ujenzi na uboreshaji wa Miundombinu ya Afya Jimboni mwetu.

### 3.1. ZAHANATI ZINAZOTOA HUDUMA ZA AFYA

Jimbo la Musoma Vijijini kwa sasa lina jumla ya Zahanati 24 za Serikali zinazotoa huduma za Afya. Zahanati ni: Zahanati ya Bugoji, Bugunda, Bukima, Busungu, Bwai, Chitare, Etaro, Kiemba, Kigera Etuma, Kiriba, Kome, Kurugee, Kwikuba, Masinono, Mwiringo, Nyakatende, Nyambono, Nyegina, Rukuba, Rusoli, Seka, Suguti, Tegeruka na Wanyere.

Zahanati 4 za binafsi zinazotoa huduma za Afya ni: Bwasi (SDA), Mji wa Huruma (Katoliki), Mugango (KMT) na Rwanga (KMT).

## 3.2. ZAHANATI MPYA ZINAZOJENGWA NA WANAVIJIJI

Wananchi wa Jimbo la Musoma Vijijini kwa kushirikiana na Serikali, Mbunge wa Jimbo, Wazaliwa wa Jimbo hili na Wadau wengine wa Maendeleo wameendelea kushiriki, kwa kasi kubwa, kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi (2015 – 2020) inayosema kwamba kila Kijiji kiwe na Zahanati yake. Utekelezaji wake ni kwa vitendo ndani ya Jimbo la Musoma Vijijini ambapo jumla ya Zahanati mpya 14 zinajengwa. Zahanati hizo ni: Burungu, Butata, Chanyauru, Chimati, Chirorwe, Kakisheri, Kurukerege, Kurwaki, Maneke, Mkirira, Mmahare, Nyambono, Nyasaungu na Nyegina. Ili kuharakisha ujenzi wa Zahanati hizo, Mbunge wa Jimbo, ameendelea kutoa MICHANGO mbalimbali kama inavyoonekana kwenye Kiambatanisho Namba 2.



*Mmoja wa Wananchi wa Kijiji cha Mkirira akimwagilia maji kwenye Boma la Zahanati ya Mkirira, Kata ya Nyegina*

## 3.3. UJENZI WA WODI ZA MAMA NA MTOTO

Zahanati 3 (Bukima, Nyegina na Kisiwa cha Rukuba) za Jimboni mwetu zimeanza ujenzi wa WODI za MAMA na MTOTO kwa lengo la kuboresha HUDUMA za AFYA zitolewazo kwenye Zahanati hizo. Prof Muhongo, Mbunge wa Jimbo la Musoma Vijijini AMEANZA KUCHANGIA ujenzi wa WODI za MAMA na MTOTO kwenye Zahanati zote tatu:

ZAHANATI ya Bukima imeshachangiwa SARUJI MIFUKO 100 bado mingine 100 itakayotolewa kulingana na kasi ya ujenzi wao.

ZAHANATI ya Nyegina imeishachangiwa SARUJI MIFUKO 50, bado SARUJI MIFUKO 150 itakayotolewa kwa utaratibu ule ule – kasi ya ujenzi.

ZAHANATI ya Kisiwa cha Rukuba imepewa SARUJI MIFUKO 50, Imebaki SARUJI MIFUKO 150. Kasi yao ya ujenzi ni kubwa.



*Mafundi wakiwa kwenye ujenzi wa WODI ya MAMA na MTOTO inayojengwakatika Zahanati ya Kijiji cha Bukima, Kata ya Bukima. Hadi sasa (Juni 30, 2020), Mbunge wa Jimbo Prof Sospeter Mwijarubi Muhongo ameishachangia SARUJI MIFUKO 100*



*Fundi akiendelea na ujenzi wa WODI ya MAMA na MTOTO kwenye ZAHANATI ya Kisiwa cha Rukuba. Hadi sasa (Juni 30, 2020), Mbunge wa Jimbo la Musoma Vijijini, Prof Sospeter Mwijarubi Muhongo ameishachangia SARUJI MIFUKO 50*

## 3.4. VITUO VYA AFYA

### 3.4.1. VITUO VYA AFYA VINAVYOTOA HUDUMA

Jimbo la Musoma Vijijini lina jumla ya Vituo vya Afya viwili vinavyotoa huduma za Afya ambavyo ni: (i) Murangi na (ii) Mugango. Vituo hivi vimejengwa kwa MICHANGO ya Wananchi kwa kushirikiana na Serikali, Mbunge wa Jimbo, Wazaliwa wa Jimbo hili na Wadau wengine wa Maendeleo.

### 3.4.2. KITUO CHA AFYA KIPYA

Serikali imetoa kiasi cha Shilingi Milioni 400 kwa ajili ya upanuzi wa Zahanati ya Masinono, Kata ya Bugwema kuwa Kituo cha Afya cha Kata hiyo. Mbunge wa Jimbo ataungana na Wananchi na Wadau wengine wa Maendeleo kuchangia ujenzi huu ili ukamilike kwa wakati na kwa ubora unaostahili. Mbunge wa Jimbo, Prof

Sospeter Mwijarubi Muhongo atachangia SARUJI MIFUKO 400 (mia nne) kwenye ujenzi huu.

### 3.4.3. HOSPITALI YA WILAYA

Wananchi na Viongozi wa ngazi mbalimbali akiwemo Mbunge wa Jimbo la Musoma Vijijini, wanaendelea kuishukuru sana Serikali chini ya Uongozi wa Rais Dkt John Joseph Pombe Magufuli kwa kutoa Shilingi Bilioni 1.8 kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali ya Wilaya inayojengwa kwenye Kitongoji cha Kwikonero, katika Kijiji cha Suguti, Kata ya Suguti. Mbunge wa Jimbo kwa kushirikiana na Wananchi wa Jimbo la Musoma Vijijini ameendelea kuchangia ujenzi huu kama inavyoainishwa kwenye Kiambatanisho Namba 2.



*Baadhi ya majengo ya Hospitali ya Wilaya ya Musoma inayojengwa katika Kitongoji cha Kwikonero, Kijijini Suguti, Kata ya Suguti*

## 4. SEKTA ZA KILIMO, UVUVI NA UFUGAJI

Mbunge wa Jimbo, Prof Sospeter Mwijarubi Muhongo kwa kushirikiana na Serikali kupitia Halmashauri ya Wilaya ya Musoma, ameendelea kuishirikisha Jamii katika kushiriki shughuli

za kiuchumi hususani za Kilimo, Uvuvi na Ufugaji ili kuimarisha kipato cha mtu mmoja mmoja na Jimbo letu kwa ujumla.

## 4.1. KILIMO

### 4.1.1. PLAU

Mbunge wa Jimbo la Musoma Vijijini, Prof Sospeter Mwijarubi Muhongo ameendelea kutekeleza Programu ya uboreshaji wa zana za Kilimo Jimboni mwetu kwa kununua Majembe ya kukokotwa na ng’ombe (PLAU) na kuyagawa bure kwenye Vikundi vya Kilimo. Programu ya kuongeza matumizi ya PLAU ndani ya Jimbo la Musoma Vijijini inaendelea kutekelezwa kwa mpangilio mzuri unaohamasisha na kuwashirikisha Wanavijiji wenyewe. Hadi kufikia Juni 2020, Mbunge wa Jimbo ameishagawa PLAU kwa Vikundi 85 vya Kilimo kutoka Vijiji vyote 68 vya Jimbo letu.



*Vikundi vya Kilimo vikipokea zawadi ya PLAU kutoka kwa Mbunge wa Jimbo la Musoma Vjijini, Prof Sospeter Muhongo (zawadi ya Sikukuu ya Eid al Fitr 2020)*

## 4.2. UVUVI

Mbunge wa Jimbo, kwa kushirikiana na Mkuu wa Wilaya ya Musoma, Dr Vincent Naano Anney na Mkurugenzi wa Halmashauri ya Musoma, Ndugu John Lipesi Kayombo wameendelea kuwashirikisha Wananchi kwenye Uvuvi Bora unaozingatia sheria, kanuni na miongozo ya Serikali. Mbunge wa Jimbo pia ameendelea kufuatilia maombi ya boti za doria yaliyoko Serikalini kwa ajili ya kuimarisha hali ya usalama ndani ya Ziwa Victoria kwa upande wa Jimbo la Musoma Vijijini.

## 4.3. UFUGAJI

Kwa kipindi hiki cha Mwaka wa Fedha 2019 - 2020, Sekta ya Ufugaji kupitia Halmashauri ya Wilaya ya Musoma imeendelea kupokea madawa ya kuogesha Mifugo (lita 50) kwa Majosho manane. Majosho hayo manane (8) ni ya Bugoji, Bugwema, Bwai Kumusoma, Chumwi, Ifulifu, Mmahare, Mugango na Saragana. Mbunge wa Jimbo, Prof Sospeter Mwijarubi Muhongo ameendelea kufuatilia maombi yaliyoko Serikalini ya kuongeza Majosho na upatikanaji wa madawa ili kukidhi mahitaji ya Wafugaji na mifugo yao.

Sekta za Kilimo, Uvuvi na Ufugaji zinatoa AJIRA za uhakika kwa VIJANA, WANAWAKE, WATU WENYE ULEMAVU na makundi mengine kwenye jamii yetu.

## 5. MAZINGIRA

Katika zoezi la kupambana na Mabadiliko ya Tabianchi, Mbunge wa Jimbo la Musoma Vijijini, Prof Sospeter Mwijarubi Muhongo kwa kushirikiana na Mkuu wa Wilaya ya Musoma, Dr Vincent Naano Anney, Mbunge wa Jimbo la Musoma Mjini, Mhe Vedastus Mathayo na Kikundi cha Wana Nyanja Development Initiative (NDI), wanaeendeleza Mradi wa uoteshaji wa Miche ya miti zaidi ya Milioni 10 na kuigawa bure kwa ajili ya kupandwa

katika Vijiji vyote vya Jimbo la Musoma Vijijini na Mitaa yote ya Manispaa ya Musoma.

## 6. UTAMADUNI NA MICHEZO

Mbunge wa Jimbo la Musoma Vijijini, Prof Sospeter Mwijarubi Muhongo ameendelea kushirikiana na Wananchi wa Wilaya ya Musoma na Mabaraza ya Wazee ya Ushauri, Ushawishi, Utamaduni na Maadili kwenye masuala ya Michezo na Utamaduni. Mbunge wa Jimbo ameendelea kutoa MICHANGO mbalimbali katika Timu za mpira wa miguu ikiwemo Timu ya Wasaga FC yenye Makao Makuu yake Kijijini Kasoma, Kata ya Nyamrandirira.

Pia, Mbunge wa Jimbo ameendeleza utaratibu wake wa KILA MWAKA wa kushindanisha Vikundi mbalimbali vya Ngoma za Asili na Kwaya pamoja na Timu za kupiga kasia. MICHANGO ya Mbunge wa Jimbo kwenye eneo hili inaonekana kwenye Kiambatanisho Namba 2.



*Timu ya Wasaga FC yenye Makao Makuu yake Kijijini Kasoma, Kata ya Nyamrandirira ikiwa katika maandalizi ya kushiriki Ligi ya Mkoa wa Mara. Mbunge wa Jimbo, Prof Sospeter Mwijarubi Muhongo amefadhili Timu hii kushiriki Mashindano ya Ligi Daraja la Tatu ngazi ya Mkoa*

## 7. MICHANGO YA WADAU WA MAENDELEO

Mbali na Wananchi, Serikali, Mbunge wa Jimbo na Wazaliwa wa Jimbo hili, Wadau wengine wa Maendeleo wameendelea kushirikiana na Serikali na Jimbo la Musoma Vijijini katika kutekeleza Miradi ya Maendeleo kwenye nyanja mbalimbali kama ifuatavyo:

### 7.1. PROJECT CONCERN INTERNATIONAL (PCI)

Hili ni Shirika la Kimataifa la Maendeleo ya Jamii (PCI, Project Concern International, USA) linalojishughulisha na utoaji wa Mafunzo ya Kilimo kwa Wananchi walio katika Vikundi ndani ya Jimbo la Musoma Vijijini na ujenzi wa vyoo vya Wanafunzi, ujenzi wa Maktaba na utoaji wa Vitabu kwa Shule za Msingi. Wananchi wa Jimbo la Musoma Vijijini wanaendelea kushirikiana na Shirika la PCI kwenye malengo yake makuu likiwemo la kutoa chakula mashuleni kupitia Vikundi vya Wakulima.

Kutokana na utoaji wa huduma ya chakula mashuleni, PCI imesaidia kuongeza hamasa kwa Wanafunzi kuhudhuria masomo na kufanya utoro Shuleni upungue, hali ambayo imepelekea kuongeza ufaulu wa Wanafunzi kwenye Mitihani yao.



*Mbunge wa Jimbo la Musoma Vijijini, Prof Sospeter Mwijarubi Muhongo (katikati mwenye kofia) akiwa na Viongozi wa PCI, Halmashauri ya Musoma na Vikundi vinavyosimamiwa na PCI kwenye Harambee ya kuchangia chakula kwa Shule za Kata ya Suguti*

## 7.2. BMZ

Mradi wa BMZ (The Federal Ministry of Economic Cooperation and Development, Germany) wa Ujerumani unatoa matibabu na huduma nyingine kwa watu wenye ulemavu kwenye Wilaya mbili za Mkoa wa Mara ambazo ni Musoma na Rorya. Kwa upande wa Wilaya ya Musoma, Mradi huu uko Jimbo la Musoma Vijijini kwenye Kata 10 ambazo ni Bugwema, Bukima, Bukumi, Bwasi, Kiriba, Makojo, Murangi, Nyambono, Nyamurandirira na Suguti.

Kama ilivyo kawaida ya BMZ, Wanafunzi wenye ulemavu wameendelea kupewa vifaa mbalimbali vya Shule vikiwemo mabegi, madaftari, kalamu na chakula (mchele, maharage na sukari). Baadhi ya Wanafunzi wenye ulemavu wamekuwa wakifanyiwa upasuaji wa marekebisho kwenye Hospitali Teule ya

Shirati. Wananchi na Viongozi wa Jimbo la Musoma Vijijini wanaendelea kushukuru sana Mradi wa BMZ (Ujerumani) kwa kutoa misaada ya vifaa, vyakula, matibabu bure na mitaji kwa watu wenye ulemavu walio kwenye Vikundi vya Jimboni mwetu.



*Baadhi ya Wanafunzi wenye ulemavu wakiwa kwenye picha ya pamoja na Walimu wao mara baada ya kupokea vifaa vya Shuleni walivyokabidhiwa na BMZ*

## 7.3. MICHANGO YA MABENKI

Mbunge wa Jimbo la Musoma Vijijini, Prof Sospeter Mwijarubi Muhongo kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Musoma na Wananchi wa Jimbo wanaendelea kuyashukuru Mashirika na Makampuni mbalimbali ya umma yaliyoko mstari wa mbele kuchangia Maendeleo ya Jimbo letu kwenye Sekta ya Elimu. Miongoni mwa Mashirika na Makampuni hayo ni Benki za CRDB, NMB, TPB na Mgodi wa Dhahabu wa Seka (MMG).



*Mkuu wa Wilaya ya Musoma, Dr Vincent Naano Anney (wa tatu kulia) akipokea vifaa vya ujenzi vilivyotolewa na Benki ya CRDB kwa ajili ya ukarabati wa Shule ya Msingi Murunyigo iliyopo Kijijini Kiemba, Kata ya Ifulifu*

## 7.4. JAMII IMPACT LIMITED

Hii ni Taasisi inayotoa Huduma ya Mikopo kwa Vikundi vinavyojishughulisha na Miradi ya kiuchumi vikiwemo VICOBA na vile vilivyo na utaratibu wa kununua hisa na kukopeshana. Vikundi kadhaa kutoka Kata za Ifulifu, Kiriba, Nyakatende, Nyambono na Suguti vimeendelea kujitokeza na kutuma maombi yao na vingine vimeanza kunufaika na mikopo ya JAMII IMPACT LIMITED. Kikundi cha TUMAINI VICOBA cha Kata ya Kiriba ni moja ya Vikundi ambavyo vimefanikiwa kukopeshwa na Jamii Impact Limited.

Jamii Impact inakaribisha Vikundi vingine kupeleka maombi yao ya MIKOPO kwenye Ofisi zao zilizopo Kijijini Nyabange kwenye Kanisa la Mennonite.

## 7.5. WADAU WENGINE WA MAENDELEO

Jimbo la Musoma Vijijini kwa kupitia Serikali ya Awamu ya Tano limeendelea kufanya kazi na Wadau mbalimbali wa Maendeleo katika Sekta za Afya, Kilimo n.k. Wadau wengine wanaoshirikiana na Wananchi wa Jimbo la Musoma Vijijini kupitia Halmashauri ya Musoma ni wafuatao:

### 7.5.1. JOHNS HOPKINS PROGRAM FOR INTERNATIONAL EDUCATION IN GYNAECOLOGYAND OBSTETRICS (JHPIEGO)

Shirika hili la nchini Marekani linajishughulisha na uboreshaji wa huduma za Afya ya uzazi kwa Mama wajawazito, uzuiaji wa saratani ya kizazi, uzuiaji wa aina tofauti ya virusi vinavyosababisha ugonjwa wa UKIMWI na utoaji huduma ya magonjwa ya kuambukiza. Ndani ya Jimbo la Musoma Vijijini, Shirika la JHPIEGO linafanya kazi katika Zahanati zote 28 zinaotoa huduma za Afya (za Serikali na Binafsi).

### 7.5.2. INTERNATIONAL CENTER OF AIDS CARE AND TREATMENT PROGRAMS (ICAP)

Hili ni Shirika la Kimataifa lenye Makao Makuu yake nchini Marekani ambalo linajishughulisha na utoaji wa Huduma ya UKIMWI katika Jamii ikiwa ni pamoja na upimaji na udhibiti wa maambukizi ya UKIMWI kwa Wasichana. Katika Jimbo la Musoma Vijijini, ICAP inafanya kazi kwenye Zahanati zote za Jimboni zinazotoa Huduma za Afya.

### 7.5.3. ARIEL GLASER PEDIATRIC AIDS HEALTHCARE INITIATIVES (AGPAHI)

Hili ni Shirika lisilo la Kiserikali linalojihusisha na utoaji wa Huduma za upimaji na udhibiti wa maambukizi ya UKIMWI kwa akina Mama na Watoto katika Zahanati zote zinazotoa Huduma za Afya ndani ya Jimbo la Musoma Vijijini. Wafadhili wa Shirika la AGPAHI ni CDC wa nchini Marekani.

### 7.5.4. AGRICULTURE FRONTIES TANZANIA (AFRO TANZANIA)

Shirika hili linafadhiliwa na Ndugu Fadhili Aboud Magaya. Makao Makuu yake yapo Kiloleni Arusha. Afro Tanzania linajishughulisha na kuwezesha kilimo cha mazao ya bustani katika Kata za Busambara, Etaro, Kiriba, Nyakatende, Nyamurandirira na Nyegina zote za Musoma Vijijini.

### 7.5.5. SWISSCONTACT

Hili ni Shirika la Kimataifa linalojishughulisha na utoaji wa vifaa na Elimu ya kilimo biashara kama vile kilimo cha mpunga na bustani kwa vijana pamoja na ufugaji nyuki katika Kata za Busambara, Mugango na Rusoli.



*Kikundi cha Wafuga Nyuki Kurwaki (KIWANYUKU) cha Kijijini Kurwaki, Kata ya Mugango kikipokea Mizinga ya kufugia nyuki kutoka Shirika la SwissContact*

**7.5.6. MEDA ECONOMIC DEVELOPMENT ASSOCIATES (MEDA)**

Ni Shirika la Kimataifa lenye malengo ya kuendeleza Jamii kwa kutatua changamoto za umaskini kwa kutumia njia za kibiashara ambazo ni endelevu. Shirika la MEDA lilianzishwa Mwaka 1953 na Kundi la Wafanyabiashara waumini wa Kanisa la Mennonite huko Waterloo nchini Canada na linashirikiana na Jamii katika kuendeleza na kukuza biashara sehemu mbalimbali Duniani bila kujali itikadi za kidini.

Shirika hili linatekeleza Miradi mbalimbali, na miongoni mwa Miradi hiyo ni Mradi wa BEST Cassava (Building an Economically Sustainable Seed System in Tanzania for Cassava). Malengo ya Mradi wa BEST Cassava ni kujenga Mfumo endelevu wa

upatikanaji mbegu bora za MIHOGO kwa njia endelevu za kibiashara, ili Wakulima waweze kupata kwa wingi mbegu bora za MIHOGO zianazokinzana na zinazostahimili magonjwa kwa wakati unaostahili na kwa bei ambayo Mkulima ataimudu.

Katika Halmashauri ya Musoma, Shirika la MEDA linafanya kazi katika Kata za Bugoji, Bukima, Kiriba, Murangi, Nyamrandirira, Rusoli na Suguti.



*Mkulima wa zao la Mihogo wa Kata ya Rusoli, Ndugu Nyabanja Juma akiwa katika Shamba Darasa analolisimamia na kulitunza*

**7.5.7. SHIRIKA LA MAENDELEO YA KILIMO NA UFUGAJI MUSOMA (SHIMAKIUMU)**

Hili ni Shirika lisilokuwa la Kiserikali, linalohudumia Wakulima, Wafugaji na Wajasiliamali wadogo wadogo. Shirika hili linafanya kazi katika Halmashauri ya Musoma kwenye Kata zote 21 za Jimbo la Musoma Vijijini.

### 7.5.8. AFRICAN INLAND CHURCH OF TANZANIA (AICT)

Ni MRADI wa Kanisa la AICT unaohusika na masuala ya kilimo na uchimbaji wa Visima vya Maji katika Kata mbili za Busambara na Tegeruka zote za Jimbo la Musoma Vijijini.

### 7.5.9. VICTORIA FARMING AND FISHING ORGANIZATION (VIFAFIO)

Ni Taasisi isiyo ya Kiserikali inayojishughulisha na uhamasishaji wa Jamii, kupinga na kutokomeza ukatili wa kijinsia katika Kata za Bukima, Bulinga, Nyamrandirira na Rusoli. Shirika hili pia linajishughulisha na uhamasishaji VICOBA, kilimo biashara (mazao ya bustani), uvuvi endelevu (ufugaji wa samaki) na utunzaji wa Mazingira (Vitalu vya Miti).

### 7.5.10. MARIE STOPES

Hili ni Shirika ambalo linafanya kazi katika nchi 37 Duniani ikiwemo Tanazania, Makao Makuu yake yapo London, Uingereza. Shirika hili linajishughulisha na utoaji wa Huduma ya Uzazi wa Mpango kwenye vituo mbalimbali vya Afya na katika maeneo ambayo ni magumu kufikika hasa ya Visiwani. Kwa upande wa Jimbo la Musoma Vijijini, MARIE STOPES inafanya kazi katika Zahanati zote 28 zinazotoa Huduma za Afya.

### 7.5.11. POPULATION SERVICES INTERNATIONAL (PSI)

Hili ni Shirika linalofadhiliwa na Global Fund lenye Makao Makuu yake nchini Marekani, Washington DC. Hutoa Huduma ya Uzazi wa Mpango na matibabu kwa Mama baada ya mimba kuharibika. Kwa upande wa Jimbo la Musoma Vijijini, Shirika hili linafanya kazi zake katika Zahanati ya Bwasi (SDA).

### 7.5.12. INTRAHEALTH INTERNATIONAL

Ni Shirika linalohusika na utoaji wa Huduma ya Tohara kwa Wanaume katika vituo vyote 28 vya kutolea Huduma za Afya. Vituo hivyo viko ndani ya Zahanati zote 28 za Jimbo la Musoma Vijijini. Makao Makuu ya Shirika hili yako Chapel Hill, North Carolina, USA.

### 7.5.13. JOHN SNOW INC (JSI)

Ni Shirika lisilo la Kiserikali la nchini Marekani, Boston ambalo kwa upande wa Tanzania linajishughulisha na uboreshaji wa mfumo wa utoaji wa Huduma za Afya na Ustawi wa Jamii. Kwa upande wa Jimbo la Musoma Vijijini, Shirika hili linafanya kazi kwenye Kata zote 21 za Jimbo la Musoma Vijijini.

### 7.5.14. CENTRE FOR WIDOWS AND CHILDREN ASSISTANCE (CWCA)

Shirika hili linalofadhiliwa na Tanzania Network for Legal Aid Providers, linajishughulisha na utoaji wa msaada wa Kisheria kwa Wanawake na Watoto kwa Kata zote 21 za Jimbo la Musoma Vijijini.

### 7.5.15. LAW SCHOOL ADMISSION COUNCIL (LSAC)

Ni Shirika linalohusika na utoaji wa msaada wa Kisheria kwa Wanawake na Watoto kwa Kata zote 21 za Jimbo la Musoma Vijijini.

### 7.5.16. CHRISTIAN COUNCIL OF TANZANIA (CCT)

Hili ni Shirika lisilo la Kiserikali la Makanisa ya ki-Protestanti linalofadhiliwa na Shirika la Maendeleo la Norway (NORAD).

Shirika hili lenye Makao Makuu yake Dodoma, linafanya kazi kupitia Mradi wa Mwanamke Jasiri (Strong Woman Program) ndani ya Jimbo la Musoma Vijijini katika Kata za Bukima, Bulinga, Busambara, Bwasi, Ifulifu, Kiriba, Makojo, Mugango, Nyamrandirira Nyegina na Tegeruka. Shirika hili linajishughulisha na mambo mbalimbali ikiwa ni pamoja na kumwezesha Mwanamke kiuchumi kwa kuwapatia mafunzo mbalimbali ya ujasiliamali, vifungashio, kuwaunganisha na Taasisi mbalimbali za Kifedha ili waweze kukopana kukuza mitaji yao. Vilevile, Shirika hili linaviwezesha Vikundi vya ujasiliamali kwenda kwenye maonyesho mbalimbali.

Pia, Shirika hili linafanya kazi ya kuhamasisha Wanawake kushiriki kwenye ngazi mbalimbali za maamuzi kwa kuwahamasisha kugombea nafasi mbalimbali za Uongozi. Vilevile, Shirika hili linafanya kazi ya kuwawezesha Wanawake kupata Elimu ya Kisheria na msaada wa Kisheria kupitia Wasaidizi wa Kisheria wanaowezeshwa na Mradi huu.



*Mkuu wa Wilaya ya Musoma, Dr Vincent Naano Anney (wa pili kushoto) akizindua Mradi wa Mwanamke Jasiri, wakati wa Maazimisho ya Siku ya Wanawake Duniani zilizofanyika Machi 12, 2019 Kijijini Kwibara Kata ya Mugango. Kulia ni Afisa Kilimo wa Wilaya ya Musoma, Ndugu Paul Makuri, akifuatiwa na Mratibu wa Mradi wa Mwanamke Jasiri Mkoani Mara, Rosemary Sendeu. Kushoto ni Mwenyekiti wa Halmashauri ya Musoma, Ndugu Charles Magoma Nyambita.*

**7.5.17. WORLD EDUCATION INC (WEI)**

Ni Shirika linalotekeleza Mradi wa Waache Wasome (Let them Learn). Mradi huu unajishughulisha na kuwajengea Wanawake uwezo wa kupata Elimu bora, kukuza kipato na ujuzi katika Kata zote 21 za Jimbo la Musoma Vijijini. WEI lenye Makao Makuu yake nchini Marekani lilianzishwa Mwaka 1951.

### 7.5.18. ONE WORLD SUSTAINABLE LIVELIHOOD (OWSL)

Ni Shirika linaloshughulika na uratibu na utekelezaji wa Taasisi za Jamii zinazolenga kuboresha Huduma za Afya ya Uzazi na Mtoto katika Jamii ya watu wa Musoma Vijijini ndani ya Kata zote 21.

### 7.5.19. CHAMA CHA UZAZI NA MALEZI TANZANIA (UMATI)

Ni Taasisi inayoshughulika na utoaji wa Huduma ya Uzazi wa Mpango na inafanya kazi katika Zahanati zote zinazotoa Huduma ya Afya ndani ya Jimbo la Musoma Vijijini.

### 7.5.20. KANISA LA KIINJILISTI LA KILUTHERI TANZANIA (K.K.K.T)

Taasisi hii pia inahusika na uhamasishaji wa Jamii kupinga na kutokomeza ukatili wa kijinsia. Vilevile, Shirika hili linashughulika na ufugaji bora wa ngombe wa maziwa. Kwenye Jimbo la Musomaa Vijijini, ni jumla ya Kata mbili za Musanja na Suguti ambazo zina Mradi wa ufugaji wa ng’ombe wa kisasa.

### 7.5.21. UMOJA WA MAENDELEO YA WATU WA BUKWAYA (UMABU)

Hii ni Taasisi inayojishughulisha na kutetea haki za watoto na kuboresha miundombinu ya Elimu kwa vijana wa kike. Makao Makuu yake yapo Kata ya Nyegina, Musoma Vijijini. Vilevile, UMABU inafanya kazi ya kuongeza uelewa katika Jamii kupitia Miradi ya Elimu na kufadhili vijana wa kike katika masomo ya Sekondari. UMABU inatekeleza Miradi yake ndani ya Kata za Etaro, Ifulifu, Nyakatende na Nyegina.

**7.5.22. MUSOMA RURAL PARALEGAL ORGANIZATION (MRPO)**

Ni Taasisi inayofanya kazi ya kutoa msaada wa Kisheria kwa watu wote wa Jimbo la Musoma Vijijini ikiwa ni pamoja na ushauri, ufafanuzi na tafsiri ya Sheria mbalimbali kama vile, urithi, mirathi, madai n.k. Makao Makuu ya Shirika hili yapo Kijijini Suguti.

**7.5.24. SUSTAINABLE HUB FOR POLICY INITIATIVES (SHPI)**

Ni Shirika lisilo la Kiserikali linalofanya kazi ya uelimishaji, utetezi wa sera na kupinga ukatili wa kijinsia (GBV) kwenye baadhi ya Kata za Musoma Vijijini ambazo ni Etaro, Bukima, Ifulifu, Kiriba, Mugango, Nyakatende, Nyegina, Suguti na Tegeruka. Wafadhili wakuu wa Shirika hili ni Foundation for Civil Society (FCS). Makao Makuu ya Shirika hili yapo Kiabakari, Wilaya ya Butiama, Mkoani Mara.

**7.5.25. WATOTO WAPINGE UKIMWI**

Hii ni Taasisi inayofadhiliwa na Shirika la Masista wa Katoliki (Maryknoll Sisters). Makao Makuu ya Shirika hili yapo nchini Marekani. Taasisi inajishughulisha na utoaji wa Elimu ya UKIMWI na kusaidia Watoto yatima wanaoishi na VVU na wale wanaoishi katika mazingira hatarishi. Kwa upande wa Jimbo la Musoma Vijijini, Taasisi hii inafanya kazi kwenye Kata za Etaro, Nyakatende na Nyegina.

**7.5.28. TANZANIA RED CROSS**

Hili ni Shirika la Msalaba Mwekundu Tanzania linalotoa Huduma ya Kwanza (First Aid) katika majanga na huduma nyingine katika matatizo mbalimbali ikiwa ni pamoja na maafa na masuala mengine

ya huduma za Afya katika maeneo yote ya Jimbo la Musoma Vijijini.

### 7.5.29. SHIRIKA LA MAENDELEO UTAFITI NA TIBA TANZANIA (SHIMAUTITA)

**SHIMAUTITA** ni Shirika lisilo la Kiserikali linalofanya kazi na baadhi ya Wilaya nchini mwetu. Makao Makuu yake yapo Nyamisisi, Kiabakari, Butiama. Kwa upande wa Jimbo la Musoma Vijijini, Shirika hili linafanya kazi ndani ya Kata zote za Jimbo la Musoma Vijijini.

Shirika hili linajishughulisha na masuala mbalimbali katika Jamii ambayo ni pamoja na utoaji wa Elimu kwa Waganga Asilia, kulinda na kutetea haki na maslahi ya Wajane.

### 7.5.30. WAZALIWA WA JIMBO LA MUSOMA VIJIJINI

Kwa kipindi chote cha Julai 2019 – Juni 2020, Mbunge wa Jimbo la Musoma Vijijini, Prof Sospeter Mwijarubi Muhongo ameendelea kuwashawishi na kuwaunganisha Wazaliwa wa Vijiji vya Jimbo hili waishio ndani na nje ya Musoma Vijijini, ili kushiriki katika shughuli za uchangiaji wa Miradi ya Maendeleo kwenye maeneo walikozaliwa.

## 8. MIRADI MINGINE YA MAENDELEO

Jimbo la Musoma Vijijini kupitia Halmashauri yake limeendelea kutekeleza na kusimamia Miradi mingi na mikubwa katika Sekta mbalimbali zikiwemo za:

## 8.1. MAJI

Serikali imeendelea kusambaza maji vijijini kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 kama ifuatavyo:

(i) RUWASA wanapanua MRADI wa MAJI ya ZIWA wa Suguti/Wanyere kwenda Saragana. Hatua iliyofikia ni ya ununuzi wa vifaa (RUWASA inazo Fedha)

### 8.1.1 MIRADI YA MAJI KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021

(ii) RUWASA watapanua MRADI huo wa MAJI ya ZIWA (Suguti/Wanyere) hadi kufika Kijijini Nyambono.

(iii) Pia, RUWASA watakuwa na MRADI MPYA wa kupeleka MAJI ya KISIMA katika Vijiji vya Bugoji na Kaburabura

(iv) Vilevile, RUWASA watafanya USANIFU wa Mradi wa MAJI ya ZIWA kuanzia Chumwi kwenda kwenye Vijiji vya Mabui Merafuru, Mikuyu na Seka.

### 8.1.2 MIRADI MINGINE YA MAJI KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021

(v) Kuchimba VISIMA na kufunga pampu za mikono katika Vijiji vya Kinyang'erere, Masinono, Muhoji.

(vi) Kupanua MRADI wa MAJI ya ZIWA wa Bulinga/Bujaga kwenda kwenye Vijiji vya Bugunda na Kome

(vii) Kupanua MRADI wa MAJI ya ZIWA wa Makojo/Chitare kwenda kwenye Vijiji vya Bwasi na Chimati

(viii) Kukamilisha ujenzi wa MRADI wa MAJI ya ZIWA wa Bulinga/Bujaga, Makojo/Chitare, Busekera, Bukima/Kwikerege, Suguti/Kusenyi na Chirorwe/Wanyere.

(ix) Kukarabati VISIMA 10 vyenye pampu za mikono

Jumla ya gharama za MIRADI yote hii ni Tsh bilioni 2.14 (RUWASA, Mwaka wa Fedha 2020/2021)

### 8.1.3 MIRADI MIKUBWA YA MAJI

### (x) Mradi wa Maziwa Makuu:

Vijiji 33 vya Jimboni mwetu vimo kwenye Mradi huu – Serikali imeshauanza na inajipanga kupata fedha za utekelezaji wake. Vijiji 33 vilivyo kwenye Mradi huu ni:

Buanga, Bugwema, Buira, Bukumi, Busamba, Busekera, Bwai Kumusoma, Bwai Kwitururu, Chumwi, Etaro, Kabegi, Kaboni, Kakisheri, Kasoma, Kastam, Kiemba, Kigera, Kinyang’erere, Kiriba, Kurukerege, Kwikuba, Lyasembe, Maneke, Masinono, Mkirira, Mmahare, Murangi, Musanja, Mwiringo, Nyegina, Rukuba, Rusoli na Tegeruka.

**(xi) Bomba kubwa la Maji la Mugango – Kiabakari –Butiama:**

Vijiji vyote vya Kata za Mugango na Tegeruka vitasambaziwa maji ya bomba hili. Fedha zipo (Saudi Arabia + BADEA + Tanzania), Wizara imetoa Tangazo la kumtafuta Mkandarasi mwingine baada ya yule wa awali kushindwa vigezo vya utekelezaji wa Mradi huu.

**(xii) Maji ya Mji wa Musoma (MUWASA)**

Hayatumiki zaidi ya 50%. Kwa hiyo, Serikali imeamua kusambaza maji hayo kwenye Vijiji jirani, vikiwemo Vijiji vyote vya Kata za Etaro, Ifulifu, Nyakatende na Nyegina. Mradi umeanza kutekelezwa.

Mbunge wa Jimbo la Musoma Vijijini, Prof Sospeter Mwijarubi Muhongo, ameendelea kuwashawishi Wananchi kuendelea

kushirikiana na Serikali kwenye utekelezaji na utunzaji wa Miundombinu ya Miradi ya Maji.

### 8.2. UMEME VIJIJINI (REA)

Serikali kupitia Wakala wa kusambaza Umeme Vijijini (REA) imeendelea na usambazaji wa umeme kwenye vitongoji ambavyo vilikuwa havijafikiwa na umeme. Lengo la Serikali ni kuhakikisha Vijiji vyote 68 na Vitongoji vyake vyote 374 vinapatiwa umeme.

### 8.3. BARABARA

#### 8.3.1. UJENZI WA BARABARA YA LAMI (TANROADS)

Ujenzi wa barabara ya Musoma – Mugango – Makojo – Busekera kwa kiwango cha lami tayari utekelezaji wake umeishaanza kwa kipande cha Km 5. Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 imeendelea kutenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa barabara hili. Wananchi wa Jimbo la Musoma Vijijini wanaendelea kuishukuru Serikali kwa kuendelea kutekeleza Ahadi za Rais wa Jamhuri ya Muungano, Mhe Dkt John Joseph Pombe Magufuli.

#### 8.3.2. MATENGENEZO YA BARABARA (TANROADS)

Jimbo la Musoma Vijijini lina barabara mbili zinazohudumiwa na TANROADS ambazo ni Musoma - Mugango - Makojo – Busekera na barabara ya Murangi – Bugwema – Manyamanyama (Bunda). Mbunge wa Jimbo anaendelea kufuatilia upatikanaji wa fedha kutoka Serikalini kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya TANROADS Jimboni mwetu.

### 8.3.3. MATENGENEZO YA BARABARA VIJIJINI (TARURA)

Serikali kupitia Wakala wa barabara Vijijini (TARURA) imetenga fedha (Tsh 300M), kwa ajili ya ujenzi wa DARAJA lililobomoka la BUKIMA – BULINGA – BWASI ambalo ni KIUNGO cha Vijiji vya Bukima, Bulinga na Bwasi. Madaraja mengine yatakayotengenezwa ni:

(i) Kataryo – Wanyere,
(ii) Kwibara – Rwamugango – Nyaminya.

TARURA imepewa zaidi ya Tsh Bilioni 1.05 kwa ajili ya utengenezaji wa barabara zetu. **SHUKRANI TELE KWA SELIKALI YETU.**

## 9. HUDUMA ZA BENKI VIJIJINI

Huduma za Benki zimeanza kushamiri ndani ya Jimbo la Musoma Vijijini ambapo Benki za CRDB na NMB tayari zina Mawakala wanaotoa huduma. Hii ni hatua muhimukabla ya ujenzi wa Matawi ya Benki hizo Jimboni mwetu. Mawakala hawa wapo katika maeneo yafuatayo:

(i) NMB - Mawakala wapo Vijijini Bukima na Mugango
(ii) CRDB - Mawakala wapo Vijijini Bukima, Mugango, Saragana na Seka
(iii) NBC – Wakala ataanzia Kijijini Murangi

Mawakala zaidi watakuwa Bwai Paris, Busekera, Etaro, Nyambono na Seka. Mbunge wa Jimbo la Musoma Vijijini Prof Sospeter Mwijarubi Muhongo anaendelea kuwashawishi Wananchi wa

Jimbo letu kutumia huduma hizi kupitia Mawakala waliopo katika maeneo yaliyotajwa.

## 10. USHIRIKI KWENYE SHUGHULI ZA CHAMA

Mbunge wa Jimbo la Musoma Vijijini, Prof Sospeter Mwijarubi Muhongo ameendelea KUCHANGIA kwa kiasi kikubwa sana Shughuli za Chama cha Mapinduzi (CCM) kuanzia ngazi ya Matawi, Kata, Wilaya, Mkoa na hata Taifa kwa ujumla. Mbunge huyu ameendelea kuchangia Vikao vyote vya Halmashauri Kuu ya Wilaya ya Musoma Vijijini, Ziara mbalimbali za Sekretarieti, ujenzi wa Ofisi ya CCM Wilaya ya Musoma Vijijini, Vifaa vya Ofisi, Mafuta kwa ajili ya Chaguzi mbalimbali za Chama, Kadi za Jumuiya na Chama, n.k. Vilevile, Mbunge huyu wa Jimbo, anaendelea kuchangia mahitaji binafsi ya Wafanyakazi wa Chama (CCM). Baadhi ya Michango hiyo imeorodheshwa kwenye Kiambatanisho Namba 2.



*Wajumbe wa Kamati ya Siasa Wilaya ya Musoma Vijijni wakikagua Mradi wa ujenzi wa Ofisi ya Chama cha Mapinduzi Wilaya ya Musoma Vijijini inayojengwa Kijijini Murangi. Mbunge wa Jimbo, Prof Sospeter Mwijarubi Muhongo hadi kufikia tarehe 6 Juni 2020, alikuwa ameishachangia jumla ya Shilingi milioni 12 (Tsh 12M)*



*Msaidizi wa Mbunge wa Jimbo la Musoma Vijijini, Ndugu Fedson Masawa (kushoto) akimkabidhi Katibu wa Chama cha Mapinduzi Wilaya ya Musoma Vijijini, Ndugu Stevene Koyo (wa pili kushoto) PRINTER iliyonunuliwa na Mbunge wa Jimbo.*

**11. KUSHIRIKIANA NA MADHEHEBU YA DINI**

Mbunge wa Jimbo la Musoma Vijijini, Prof Sospeter Mwijarubi Muhongo ameendelea kuungana pamoja na Waumini wa Madhehebu mbalimbali wakiwemo Waislamu na Wakristu katika kuazimisha Sikukuu zao zinazotambulika kwa mujibu wa imani zao. Miongoni mwa Sikukuu hizo ni pamoja na Mfungo wa Mwezi Mtukufu wa Ramadhan na Sikuku ya Idd al Fitr (Waislam), Pasaka na Krismasi (Wakristu).

Kutokana na maradhi ya KORONA (Covid - 19), Mbunge wa Jimbo ametumia Sherehe za Idd al Fitr za mwaka huu kugawa bure Majembe (PLAU) kwa Vikundi 45 badala ya kushiriki chakula cha pamoja kama ilivyozoeleka.

## 12. USHIRIKI KWENYE MASUALA YA KIJAMII

Mbunge wa Jimbo ameendelea kuwa mstari wa mbele katika kuguswa na kushirikiana na Jamii ya Jimbo la Musoma Vijijini hasa katika matatizo mbalimbali kama ya maafa, ugonjwa na misiba. Kwenye matatizo haya Mbunge wa Jimbo amekuwa akichangia michango mbalimbali ikiwemo ya chakula, matibabu, usafiri n.k.

## 13. HITIMISHO

Kwa kipindi chote cha Julai 2019 – Juni 2020, Jimbo la Musoma Vijijini linmeendelea kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi (CCM) ya Mwaka 2015 – 2020 kwa MAFANIKIO MAKUBWA sana. Mafanikio haya yanatokana na Wananchi Vijijini kukubali kujitolea kutekeleza Miradi ya Maendeleo iliyobuniwa na kuasisiwa na wao wenyewe wakishirikiana na Serikali yao.

Miradi ya Maendeleo ya Jimbo la Musoma Vijijini kwenye Sekta za Elimu, Afya, Kilimo (Ufugaji na Uvuvi), Mazingira, Michezo na Utamaduni, imetayarishwa na kutekelezwa kwa kuzingatia Ilani ya Uchaguzi ya CCM (2015 – 2020). Miradi ya usambazaji wa umeme, maji na miundombinu ya mawasiliano nayo ni sehemeu ya utekelezaji wa Ilani hii ya CCM.

Ahadi zote za Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi (CCM) Taifa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe Dkt John Joseph Pombe Magufuli alizotoa kwa Wananchi wa Jimbo la Musoma Vijijini zinaendelea kutekelezwa ikiwemo ya ujenzi kwa

kiwango cha lami, barabara ya Musoma – Mugango – Makojo – Busekera. Ahadi nyingine za Viongozi wa Chama cha Mapinduzi (CCM) na Serikali wa ngazi mbalimbali nazo zimeendelea kutekelezwa kwa kasi ya kuridhisha.

Mbunge wa Jimbo la Musoma Vijijini, Prof Sospeter Mwijarubi Muhongo anaendelea kushirikiana vizuri sana na Wananchi Vijijini, Viongozi wa Chama na Serikali wa ngazi zote kutekeleza kwa mafanikio makubwa Ilani ya Uchaguzi ya CCM (2015 – 2020). Mbunge huyu wa Jimbo la Musoma Vijijini ameendelea kutoa MICHANGO mingi na mikubwa kwenye Miradi yote ya Maendeleo kwenye Vijiji vyote 68 na Kata zote 21 za Jimbo la Musoma Vijijini. Ahadi za Mbunge wa Jimbo zimetekelezwa na kuvuka malengo yaliyowekwa hapo awali.

## 14. SHUKRANI

Mbunge wa Jimbo la Musoma Vijijini, Prof Sospeter Mwijarubi Muhongo anaendelea kutoa Shukrani nyingi kwa Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi (CCM) Taifa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe Dkt John Joseph Pombe Magufuli, Mwenyekiti wa CCM na Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Mhe Dkt Ali Mohamed Shein, Makamu Mwenyekiti wa CCM Tanzania Bara, Mhe Philipo Mangula na Katibu Mkuu wa CCM Taifa, Dkt Bashiru Ally kwa usimamizi wao thabiti wa utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi (CCM) ya 2015 – 2020.

Mbunge wa Jimbo, kwa niaba ya Wananchi wa Jimbo la Musoma Vijijini anaendelea kutoa Shukrani nyingi kwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe Samia Suluhu Hassan, Waziri Mkuu Mhe Kasim Majaliwa Kasim, Waheshimiwa Mawaziri, Manaibu Waziri, Makatibu Wakuu na Viongozi wote wa Serikali kwa ushirikiano mkubwa wanaoendelea kuutoa katika kuunga mkono jitihada za Wananchi wa Jimbo la Musoma Vijijini kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya CCM 2015 - 2020.

Mbunge wa Jimbo, Prof Sospeter Mwijarubi Muhongo anatoa Shukrani zake za dhati kwa Mkuu wa Mkoa wa Mara, Mhe Adam Malima, Mkuu wa Wilaya ya Musoma, Mhe Dr Vincent Naano Anney na Wafanyakazi wote wa Mkoa wa Mara kwa jitihada na ushirikiano mzuri wanaoutoa katika kutekeleza Miradi ya Maendeleo kwenye Vijiji vyote 68 na Kata zote 21 za Jimbo la Musoma Vijijini.

Shukrani nyingi pia zinatolewa kwa Uongozi wa Chama cha Mapinduzi (CCM) na Jumuiya zake kwa ngazi zote tokea Tawi, Kata, Wilaya, Mkoa hadi Taifa. Shukrani za kipekee zinatolewa kwa Mlezi wetu ki-Chama (CCM) wa Mkoa, Ndugu Kheri James, Mwenyekiti wa CCM Mkoa, Ndugu Samweli Kiboye, Katibu wa CCM Mkoa wa Mara, Ndugu Shaibu Ngatiche, MNEC Mkoa wa Mara, Ndugu Christopher Gachuma, Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Musoma Vijijini, Ndugu Nyabukika Bwire Nyabukika, Katibu wa CCM Wilaya ya Musoma Vijijini, Ndugu Peter Francis Mashenji (na mtangulizi wake Ndugu Steven Koyo) na

Wafanyakazi wengine wote wa CCM na Jumuiya zake wa ngazi zote.

Shukrani zinatolewa kwa Waheshimiwa Madiwani wa Halmashauri ya Wilaya ya Musoma wakiongozwa na Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo Mhe Charles Magoma Nyambita, kwa kusimamia vizuri Miradi ya Maendeleo inayotekelezwa kwenye Kata zao. Madiwani hawa wanatoa ushirikiano mzuri sana kwa Mbunge wa Jimbo na Wasaidizi wake watatu (Ndugu Fedson Masawa, Hamisa Gamba na Verediana Mgoma).

Aidha, Mbunge wa Jimbo, anatoa Shukrani nyingi kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Musoma, Ndugu John Lipesi Kayombo, Wakuu wote wa Idara za Halmashauri ya Musoma, Watendaji wote ngazi ya Kata na Vijiji kwa jitihada zao za usimamiaji mzuri wa Miradi ya Maendeleo ya Jimbo la Musoma Vijijini. Wafanyakazi wote wa Halmashauri yetu wanapewa Shukrani za dhati kwa kutimiza wajibu wao wenye mafanikio makubwa.

Mbunge wa Jimbo, anamshukuru Ndugu Isack Kambira, Mtendaji Mkuu (Webmaster) wa Tovuti ya Jimbo la Musoma Vijijini kwa kuhakikisha taarifa za Maendeleo ya Jimbo zinawafikia Wananchi ndani ya Jimbo la Musoma Vijijini, Mkoa, Taifa na Ulimwenguni kote. Ndugu Kingi Imani na Ndugu Riadha Saidi wanapewa Shukrani nyingi kwa kusambaza taarifa za Maendeleo ya Jimbo la Musoma Vijijini kupitia Redio ya Mtandaoni inayojulikana kwa jina la “Musoma Vijijini Online Redio”

Shukrani za pekee zinatolewa kwa Wasaidizi wa Mbunge wa Jimbo la Musoma Vijijini, Ndugu Fedson Masawa, Verediana Mgoma na Hamisa Gamba kwa jitihada zao wanazozifanya na kufanikisha kwa kiasi kikubwa kufuatilia, na kutoa taarifa za mara kwa mara za Maendeleo ya Jimbo. Vilevile, Wasaidizi hawa wa Mbunge wa Jimbo wamefanikiwa kuwafikia Wananchi Vijijini mwao na kupokea kero zao bila wao (wanavijiji) kutumia gharama zao kusafiri kwenda kwenye Ofisi ya Mbunge.

Mbunge wa Jimbo hili, Prof Sospeter Mwijarubi Muhongo kwa niaba ya Wananchi wa Jimbo la Musoma Vijijini, anawashukuru Wadau mbalimbali wa Maendeleo, kwa MICHANGO yao wanayoendelea kutoa ili kufanikisha Miradi ya Maendeleo ya Sekta mbalimbali. Wadau hao ni pamoja na: Afro Tanzania, AGPAH, AICT, BMZ, CRDB, EP4R, EQUIP, ICAP, Jamii Impact Limited, JHPIEGO, Madhehebu ya Dini, MEDA, MGODI wa Dhahabu wa Seka (MMG), NMB, NSSF, PCI, SHIMAKIUMU, SwissContact, TBP na Wazaliwa wa Jimbo la Musoma Vijijini waishio ndani na nje ya Jimbo. Serikali za Australia, China, Japan, Korea Kusini, Marekani (USA), Uingereza na Ujerumani zinatambuliwa kwa Misaada yao kwa Jimbo letu.

Shukrani nyingine zinatolewa kwa Vyombo vya Ulinzi na Usalama vya Mkoa wa Mara na Wilaya ya Musoma chini ya Mkuu wa Mkoa wa Mara, Mhe Adam Malima na Mkuu waWilaya ya Musoma, Mhe Dr Vincent Naano Anney kwa kuhakikisha Wananchi wa Mkoa wa Mara hususani wa Wilaya ya Musoma (na mali zao)

wanaishi kwa usalama, amani na utulivu kwa manufaa ya Maendeleo ya Jimbo, Wilaya yetu na Mkoa kwa ujumla.

Shukrani za pekee kabisa ziwaendee Wananchi wote wa Jimbo la Musoma Vijijini wa Kata zote 21, Vijiji 68 na Vitongoji vyote 374 kwa ushirikiano mkubwa wanaoutoa katika kujitolea kuchangia shughuli mbalimbali za Maendeleo ndani ya Jimbo letu. Wazee wa Mabaraza ya Ushauri, Ushawishi, Utamaduni na Maadili ya Kata zote 21 na Vijiji 68 wanapewa shukrani nyingi kwa kushawishi na kuhimiza utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi (2015 – 2020) ndani ya Jimbo la Musoma Vijijini kwa mafanikio makubwa.

**KUPITIA CCM**

**TUTAVUKA**

**TUTAFANIKIWA**

**KIAMBATANISHO NAMBA 2:**

Orodha ya MICHANGO ya Mbunge wa Jimbo la Musoma Vijijini, Prof Sospeter Mwijarubi Muhongo kwa kipindi cha Julai 2019 – Juni 2020.

| **KIJIJI** | **TUKIO** | **MICHANGO** |
|---|---|---|
| Musoma Vijijini | Kuchangia ujenzi wa Ofisi ya CCM Wilaya (Kijijini Murangi) | Milioni 12 Ataendelea kuchangia |
| Musoma Vjijini | Kuchangia Ziara za Sekretarieti ya Wilaya | Chakula, Malazi na Mafuta |
| Musoma Vijijini | Kununua Kadi za Jumuiya ya Wazazi | Kadi 1,000 |
| Musoma Vijijini | Kuchangia PRINTER kwa ajili ya shughuli za Ofisi ya Chama cha Mapinduzi, Musoma Vijijini | Printer 1 |
| Musoma Vijijini | Kuchangia Maandalizi ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa (usafiri) | Mafuta lita 400 |
| | Kuchangia Vikao vyote vya Halmashauri Kuu ya CCM Wilaya ya Musoma Vijijini | Nauli kwa Wajumbe wote 110 |
| Musoma Vijijini | Kununua Plau 85 na kugawia Vikundi vya Kilimo | Tsh. 9,350,000/= |
| Musoma Vijijini | Kusafirisha Kikundi cha LIRANDI cha Kata ya Bugwema kwenda kushiriki “Tulia Traditional Dances Festival”, Tukuyu, Mbeya | Nauli, chakula na malazi |
| Butiama | Kuchangia Maandalizi ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa | Mafuta lita 300 |

| | | |
|---|---|---|
| Mkoa wa Mara | Kuchangia Mafuta kwa ajili ya Ziara za Viongozi wa Mkoa kwenye shughuli za Uchaguzi wa Serikali za Mitaa | Mafuta lita 200 |
| | Kulipia gharama ya kusafirisha Vijana Chipukizi (CCM) kutoka Dodoma kurudi Mkoani Mara | Tsh. 750,000/= |
| Suguti | Kugharamia Mashindano ya Nanenane | Zawadi, Nauli kwa Vikundi vya Ngoma na Kwaya.<br>Nauli kwa Madiwani na Viongozi wa CCM.<br>Chakula kwa Vikundi vyote, Viongozi na Wananchi, Muziki, Viti, Mahema |
| Busamba | Kuchangia Kikao cha kujadili na kugawa Fedha za Mfuko wa Jimbo (Tsh 53.8) Milion | Nauli kwa Viongozi wa CCM na Madiwani |
| Butiama | Kuchangia Mjadala juu ya FALSAFA ya Baba wa Taifa kuhusu Maendeleo Vijijini | Usafiri, malazi na chakula kwa Vikundi 2 |
| | Kuchangia Maazimisho ya Miaka 20 ya Kifo cha Baba wa Taifa | Chakula na maji kwa Wageni, Chakula na malazi kwa baadhi ya Wajumbe wa Jumuiya ya |

| | | |
|---|---|---|
| | | UVCCM Taifa |
| Halmashauri | Kuchangia kikao cha kugawa vifaa vilivyonunuliwa kwa Fedha za Mfuko wa Jimbo la Musoma Vijijini<br>(Saruji Mifuko 1,052; Mabati 1,080; Nondo 200 | Nauli kwa Viongozi wa CCM na Madiwani |
| Tegeruka | Kuchangia ujenzi S/M Nyaminya A&B | Saruji Mifuko 100 Milango 2 |
| Suguti | Kuchangia ujenzi wa Hospitali ya Wilaya inayojengwa Suguti | Saruji Mifuko 100 |
| Chumwi | Kugharamia Uzinduzi wa Kitabu cha Taarifa ya Utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM (2015 - 2020), Vitabu 5,000 | Nauli kwa Viongozi wa CCM wa Taifa, Mkoa, Wilaya, Kata na Matawi |
| Tegeruka | Kugawa Vitabu vya Taarifa ya Utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM (2015 - 2020) na kuhamasishaji Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, Vitabu 400 | Nauli kwa Viongozi wa CCM wa Kata na Matawi |
| Maneke | Kugawa Vitabu vya Taarifa ya Utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM (2015 - 2020) na kuhamasishaji Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, Vitabu 350 | ……..//……….. |
| Bukumi | Kugawa Vitabu vya Taarifa ya Utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM (2015 - 2020) na kuhamasishaji Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, Vitabu 300 | ……..//……….. |

| | | |
|---|---|---|
| Makojo | Kugawa Vitabu vya Taarifa ya Utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM (2015 - 2020) na kuhamasishaji Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, Vitabu 350 | ……..//……….. |
| Bwasi | Kugawa Vitabu vya Taarifa ya Utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM (2015 - 2020) na kuhamasishaji Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, Vitabu 250 | ……..//……….. |
| Bulinga | Kugawa Vitabu vya Taarifa ya Utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM (2015 - 2020) na kuhamasishaji Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, Vitabu 300 | ……..//……….. |
| Bwai Kwitururu | Kuzindua Kampeini za Uchaguzi wa Serikali za Mitaa Katani Kiriba, Vitabu 500 | ……..//……….. |
| Masinono | Kugawa Vitabu vya Taarifa ya Utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM (2015 - 2020) na kuhamasishaji Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, Vitabu 150 | ……..//……….. |
| Nyambono | Kugawa Vitabu vya Taarifa ya Utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM (2015 - 2020) na kuhamasishaji Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, Vitabu 200 | ……..//……….. |
| Rusoli | Kugawa Vitabu vya Taarifa ya Utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM (2015 - 2020) na | ……..//……….. |

| | | |
|---|---|---|
| | kuhamasishaji Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, Vitabu 150 | |
| Musanja | Kugawa Vitabu vya Taarifa ya Utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM (2015 - 2020) na kuhamasishaji Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, Vitabu 100 | ……..//……….. |
| Lyasembe | Kugawa Vitabu vya Taarifa ya Utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM (2015 - 2020) na kuhamasishaji Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, Vitabu 100 | ……..//……….. |
| Seka | Kugawa Vitabu vya Taarifa ya Utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM (2015 - 2020) na kuhamasishaji Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, Vitabu 300 | ……..//……….. |
| Kusenyi | Kugawa Vitabu vya Taarifa ya Utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM (2015 - 2020) na kuhamasishaji Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, Vitabu 250 | ……..//……….. |
| Kusenyi | Kugawa Vitabu vya Taarifa ya Utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM (2015 - 2020) na kuhamasishaji Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, Vitabu 200 | ……..//…..….. |
| Wanyere | Kugawa Vitabu vya Taarifa ya Utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM (2015 - 2020) na kuhamasishaji Uchaguzi wa | ……..//……….. |

| | | |
|---|---|---|
| | Serikali za Mitaa, Vitabu 150 | |
| Suguti | Kugharamia Kikao cha Wazee wa Mabaraza kwenye Kikao cha tathimini ya mwaka 2019 ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo Vijijini mwetu | Chakula na nauli za Wajumbe kutoka Kata 21 |
| Mwiringo | Kuchangia Sherehe ya Miaka 50 ya Shule ya Msingi Mwiringo | Chakula (ng'ombe na mchele) Ahad: Saruji Mifuko 50 (wakiwa tayari) |
| Chumwi | Kununua na kugawa Zawadi ya Plau kwa Vikundi 12 kutoka Vijiji 12 | Plau 12 |
| Kusenyi | Kununua na kugawa Zawadi ya Plau kwa Vikundi 38 kutoka Vijiji 38 | Plau 38 |
| Kwibara | Kununua na kugawa Zawadi ya Plau kwa Vikundi 15 kutoka Vijiji 15 | Plau 15 |
| Kabegi | Kununua na kugawa Zawadi ya Plau kwa Vikundi 6 kutoka Vijiji 6 | Plau 6 |
| Mkirira | Kununua na kugawa Zawadi ya Plau kwa Vikundi 14 kutoka Vijiji 14 | Plau 14 |
| Nyasaungu | Kuchangia Sherehe ya Krismasi katika Kanisa la PEFA | Chakula na maji |
| | Kuchangia ujenzi wa Zahanati ya Kijiji cha Nyasaungu | Nondo 20 |
| | Kuchangia ujenzi wa Sekondari | Ahadi: Mabati 54 |

| | | |
|---|---|---|
| | ya Nyasaungu | (wakiwa tayari) |
| Bukima | Kugharamia Mashindano ya Kupiga Kasia | Nauli kwa Viongozi wa CCM na Madiwani, Zawadi (fedha taslim) na Vikombe kwa Washindi 3 |
| Kwikuba | Kuchangia ujenzi wa Vyumba vya Madarasa katika Sekondari mpya ya Busambara | Rangi ya kupaka Vyoo 3 na Ofisi ya Utawala |
| Bulinga | Kuchangia ujenzi wa Vyumba vya Madarasa ya Shule ya Sekondari Bulinga | Saruji Mifuko 35 |
| Nyakatende | Kuchangia Harambee ya kukamilisha ujenzi wa chumba kipya kimoja (1) cha darasa katika Sekondari ya Nyakatende | Ahadi: Saruji Mifuko 50 na Mabati 27 (wakiwa tayari) |
| Rusoli | Kuchangia Kikao cha kukabidhi vifaa katika Shule 3 za Kata ya Rusoli kwa niaba ya kikundi cha YEBHE CHIKOMESHE na kushiriki Harambee ya ujenzi wa Vyumba vya Madarasa | Ahadi: Saruji Mifuko 50 (wakiwa tayari), Nauli kwa Viongozi wa CCM |
| Bukima | Kuchangia Sherehe za uzinduzi wa Shule ya Msingi Agape na kuweka Jiwe la Msingi katika jengo la TEHAMA | Vitabu, Saruji Mifuko 50, Ngano Kg 25 na Sukari Kg 25 Ahadi: Kompyuta 1 na Printer 1 |

| | | |
|---|---|---|
| | | (wakiwa tayari) |
| Kasoma | Kuifadhili Timu ya WASAGA FC | Usajili wa Wachezaji, jezi mpya na viatu vipya vya Wachezaji |
| Bugoji | Kugharamia Tafrija ya ukamilishaji wa ujenzi wa Sekondari ya Dan Mapigano Memorial | Chakula (mchele, ng'ombe na mafuta) |
| Kwikuba | Kugharamia Tafrija ya ukamilishaji wa ujenzi wa Sekondari ya Busambara | Chakula (mchele, ng'ombe na mafuta), Kibao cha Jiwe la Msingi na Uzinduzi |
| Kabegi | Kuchangia ujenzi wa Sekondari mpya ya Ifulifu | Saruji Mifuko 50 |
| Nyegina | Kuchangia ujenzi wa Jengo la Mama na Mtoto katika Zahanati ya Nyegina | Saruji Mifuko 200 (wameanza kuchukua Mifuko 50) |
| Rukuba | Kuchangia ujenzi wa Jengo la Mama na Mtoto katika Zahanati ya Rukuba Kisiwani | Saruji Mifuko 200 (wameanza kuchukua Mifuko 50) |
| Kiriba | Kuchangia ujenzi wa Vyumba vya Madarasa na ukamilishaji wa Maabara katika Shule ya Sekondari Kiriba | Saruji Mifuko 175 |
| Bugoji | Kuchangia mbao kwa ajili ya | Tsh. 1,925,000/= |

| | | |
|---|---|---|
| | utengenezaji wa meza na viti katika Sekondari ya Dan Mapigano Memorial | |
| Kwikuba | Kugharamia Kikao cha Watendaji wa Kata (WEOs) ili kujadili utekelezaji wa Miradi ya Kata zao | Nauli |
| Kome | Kuchangia ujenzi wa Vyumba vya Madarasa katika Sekondari ya Nyanja | Mabati 54 |
| Butata | Kuchangia ujenzi wa vyumba vya Madarasa katika Shule ya Msingi Butata | Saruji Mifuko 100 |
| Nyamrandirira | Kuchangia ujenzi wa Sekondari mpya ya Seka | Saruji Mifuko 250 |
| Buraga | Kuchangia ujenzi wa Shule Shikizi ya Buraga Mwaloni | Saruji Mifuko 50 |
| Chirorwe | Kushiriki Harambee ya uchangiaji wa chakula cha Wanafunzi wa Shule mbili za Chirorwe na Sokoine na nyingine nane za Kata ya Suguti | Magunia 11 ya mahindi, maharage magunia 2.75 |
| Kiriba | Kuchangia ujenzi wa Vyumba vya Madarasa katika Shule ya Msingi Nyamiyenga | Saruji Mifuko 100 |
| Lyasembe | Kuchangia ujenzi wa Vyumba vya Madarasa katika Shule ya Msingi Murangi B | Saruji Mifuko 50 |
| Kurwaki | Kuchangia ujenzi wa Vyumba vya Madarasa katika Shule ya Msingi Karubugu | Saruji Mifuko 50 |

| | | |
|---|---|---|
| Kabegi | Kuchangia ujenzi wa Sekondari ya Kata ya Ifulifu | Matofali 500 |
| Nyasaungu | Kuchangia ujenzi wa Sekondari ya Nyasaungu | Matofali 500 |
| Butiama | Kulipia gharama za kukarabati Kaburi la Baba wa Taifa (kupaka rangi) | Tsh. 279,000/= |
| Butiama | Kusafirisha Kikundi cha EGUMBA kwenda kushiriki Mashindano ya Kimataifa ya Ngoma za Asili Jijijini Dar es Salaam | Nauli, chakula na malazi |

**….. UTEKELEZAJI WA ILANI YA CCM KWA VITENDO….**



……………………………………………

**Prof Dr.rer.nat. Sospeter M Muhongo (MP)**

***(Officier, Ordre Palmes Academiques)***

***FGSAf, FAAS, MASSAF, FASI, FASSAf, FTAAS, FGIGE,***

***FTWAS, HonRFCAGS, HonFGSA, HonFGS, CGeol, EurGeol***

**Juni 30, 2020**